



**CHAMA CHA WANASHERIA WATETEZI
WA MAZINGIRA (LEAT)**

NA

**UTEKELEZAJI WA KAMPENI YA
MAENDELEO YA SEKTA YA KILIMO
TANZANIA**



*Kimeandaliwa na,
Chama Cha Wanasheria Watetezi wa
Mazingira
Jengo la Mazingira, Mtaa wa Mazingira,
Eneo la Mikocheni 'B'
S.L.P. 12605,
Dar es Salaam.
Simu/Nukushi: 255-2780859/2781098
Barua pepe: info@leattz.org
Tovuti: www.leat.or.tz*

*Na kufadhiliwa na **Trust Africa.***



*"Ongezeko la Bajeti ya Kilimo, Maendeleo ya
Kilimo, Ustawi wa wakulima"*





KUHUSU LEAT

Neno LEAT ni kifupisho cha maneno ya Kiingereza 'Lawyers' Environmental Action Team' ambayo kwa Kiswahili ni 'Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira'. LEAT ni Taasisi ya Kiraia iliyoanzishwa mnamo mwaka 1994 na kusajiliwa rasmi mwaka 1995 kama Taasisi isiyokuwa ya Kiserikali yaani 'Non Governmental Organization' (NGO). Novemba 2001 LEAT ilisajiliwa tena kama Kampuni isiyokuwa na Mtaji wa Hisa chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002.

Dhamira ya LEAT

Dhamira ya Kuanzishwa kwa LEAT ilikuja baada ya Wanasheria waanzilishi kugundua kuwa Sheria ni chombo muhimu cha kulinda Mazingira na usimamizi mzuri wa Maliasili za Taifa. LEAT ni Taasisi ya kwanza yenye kusimamia Sheria za Mazingira kwa maslahi ya Umma Kuanzishwa nchini Tanzania. LEAT inafanya tafiti za kisera na Kisheria, Ushawishi kwa masuala mbalimbali yenye maslahi ya Umma, na kufungua na kusimamia kesi zenye masilahi ya Umma kwa niaba ya Wananchi au Mazingira.

Dira ya LEAT

"Afrika yenye Mazingira na Maliasili endelevu zinazosimamiwa vizuri kwa vizazi vilivyopo na vijavyo"

Dhima ya LEAT

Kuchangia katika utawala bora wa Matumizi na usimamizi endelevu wa Mazingira na maliasili kwa njia ya kufungua na kusimamia kesi zenye masilahi ya Umma, kufanya ushawishi, kufanya tafiti za kimkakati, kuwajengea uwezo wananchi na kufanya kazi kwa mitandao.

Maadili Muhimu

LEAT itaendelea kujihusisha kikamilifu katika kusimamia maadili yafuatayo:-

- Uaminifu
- Nidhamu ya kweli
- Kufanya kazi kwa pamoja na kujitolea
- Kutetea usalama wa Mazingira
- Mwitikio wa wakati na Ufahamu
- Kuheshimu Haki za binadamu
- Uwazi na Uwajibikaji

LEAT NA UTEKELEZAJI WA MRADI WA USHAWISHI KWA MAENDELEO YA SEKTA YA KILIMO

Chama cha Wanasheria Watetezi wa Mazingira (LEAT), kwa ufadhili wa Trust Africa kinatekeleza mradi wa ushawishi kwa serikali wenye lengo la kuleta maendeleo katika sekta ya Kilimo kupitia Bajeti ya Serikali. Kampeni hii ina lengo la kuhakikisha Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania inatimiza maazimio iliyoingia kitaifa

na kimataifa yenye lengo la kuendeleza sekta ya kilimo. Maeneo ya ushawishi kwa Kampeni hii yametolewa katika maazimio na matamko yafuatayo ya Programu Kabambe ya Kuendeleza Kilimo Afrika (CAADP) na Tamko la Maputo la mwaka 2003. Mambo makuu matatu ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia kuyatimiza ni:-

- i. Kuongeza Bajeti ya sekta ya kilimo mpaka kufikia angalau asilimia 10 ya Bajeti ya Serikali hadi kufikia mwaka 2010.
- ii. Kuhakikisha sehemu kubwa ya Bajeti iliyotengwa inaelekezwa katika Maendeleo (Angalau 50/50 Maendeleo na Uendeshaji) na kulenga kuwaendeleza wakulima wadogo.
- iii. Kuhakikisha ukuaji wa sekta ya kilimo unaongezeka hadi kufikia asilimia 6.

Endapo Tanzania itafikia Maazimio haya itakuwa imepiga hatua nzuri kwa katika vitendo kufikia Malengo ya Millennium, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Kukuza Uchumu na Kuondoa Umasikini Tanzania (MKUKUTA I & II).